

fedha 2020/21 kutoka Shirika la Nyumbu Tanzania (TATC).

bungeni jana wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Magu, Boniventura Kiswaga (CCM) aliy-

fedha 2022/23 Tanroad Mkoa wa Mwanza wamepanga kuweka taa katika miji ya Magu, Kisesa na

waweze kutimbia taa katika miji ya kuweka taa kwenye miji yao," alisema Kasekenya.

miogoro ya miji ya Mwanza Juni, mwaka huu," alisema Dk Molel.

# \* Serikali yahimiza kutenga ardhi ya wafugaji, wakulima \*

**S**ERIKALI itaendelea kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji nchini ili kuwe na maeneo mahususi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Matumizi mengine ya ardhi ni pamoja na kutunza vyanzo vya maji ili kukabili-ana na migogoro ya wafugaji na wakulima nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamise-mi), Festo Dugange alisema hayo bungeni jana wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Francis Ndulane (CCM).

Katika swali lake, Ndulane alitaka kujua lini serikali itatekeleza Mpango

wa Matumizi Bora ya Ardhi ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kilwa.

Alisema katika Halmashauri ya Kilwa, serikali imetenga bajeti ya Sh milioni 60 kwa ajili ya kupitia mipango bora ya ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa yenye vijiji 90 am-

bavyo kati ya hivyo vijiji 56 vina mpango wa matumizi bora ya ardhi mpaka kufikia mwaka wa fedha 2021/22.

"Ili kuondoa na kumaliza kabisa migogoro ya wakulima na wafugaji serikali imejipanga kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji sita kwa kila mwaka.

"Kwa mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga fedha hizo kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji vya Nandete, Kiranjeranje na Ruhatwe," alisema Dugange.

Alizielekeza halmashauri na wilaya zote nchini kutenga fedha kila mwaka

katika bajeti zao kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo yote ya vijiji.

Pia, alizitaka kuweka alama zinazoonekana kwa urahisi ili kuwezesha maeneo hayo kulindwa na kuzuia mwingiliano wa kimatumizi unaofanywa na wananchi.

# Wakulima waishukuru serikali soko la mwani

Na Sijawa Omary, Mtwara

**W**AKULIMA wa mazao ya bahari, hususani mwani katika Kijiji cha Mnazi Kata ya Nalingu Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, wameishukuru serikali kwa kuwaboresha bei ya soko la bidhaa hiyo kutoka Sh 500 ya awali hadi kufikia Sh 2,000 kwa sasa.

Mmoja wa wakulima hao, Tuka Bakari alisema awali zao hilo lilikuwa na changamoto kutokana na bei kuwa ndogo ikilinganishwa na sasa hali ambayo inaleta hamasa na tija kubwa kwa wakulima.

Kwa mujibu wa Bakari, siku za nyuma, bei ya mwani ilikuwa Sh 500 kwa kilogramu na sasa imepanda hadi Sh 2,000 kwa kilogramu moja.

"Kusema ukweli hali ya bei ya sasa hivi inatupa hamasa na tumehamasika na kuongeza bidii kwenye uzalishaji kwa sababu maslahi yake tunayaona," alisema Bakari.

Alisema kilimo cha mwani kimekuwa kikiwanufaisha zaidi wanawake kwa sababu wakienda baharini kuvuna, wanapopata fedha baada ya mauzo, huzitumia kuendeshea maisha yao ya kila siku.

Siwema Mohamed alisema licha ya serikali kuboresha soko hilo, kwa sasa lakini pia mazingira ya kuuza yamekuwa rafiki ikilinganishwa na zamani ambapo ilikuwa mpaka wajikusanye kwa wingi ndipo wafanye biashara tofauti na sasa.

Alisema hali ya soko si mbaya kwa sababu zamani alikuwa akinunua mtu mmoja lakini sasa wanunuzi wameongezeka.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mnazi, Mfaume Hamisi alisema kupanda kwa bei ya zao hilo kumekuwa msaada kwa wakulima hao kwa kuwa sasa wanaweza kupata fedha za kutosha endapo watakuwa na dhana ya kutanua wigo kwenye maeneo ya mashamba yao.

CC

Na Mw Zanzib:

C  
taka vi  
kuhaki  
utekele  
hicho, i  
kimkal  
serikal  
Hay  
nyekiti  
Kusini  
alipozu  
viongo:



S

Na J

S

maji  
una  
ya t  
Mb  
M  
Jum  
kati  
wa  
leng  
ya l